COVID-19 GUIDANCE


# Covid-19
# Mwongozo wa kanisa la nchini

Covid-19 imesababisha makanisa kuuliza maswali mengi ulimwenguni kote. Hati hii inatoa mwongozo kwa kanisa kukabiliana na janga hili.

Virusi vya Covid-19 huenezwa na watu waliokaribiana (chini ya mita 2) kwa kuwa matone husambazwa kati yao, hasa kwa kukohoa na kupiga chafya. Pia husambazwa kupitia mgusano wa mwili wakati watu wanagusa vitu vilivyoambukizwa kisha kugusa mdomo, macho au pua lao au kugusana wenyewe kwa mikono isio safishwa.

Dalili zinajumuisha:

- homa na uchovu
- kukohoa kwa muda mrefu
- matatizo ya kupumua




tearfund.org/covid19
covid19-response-team@tearfund.org



Registered office: 100 Church Road, Teddington TW11 8QE. Registered in England: 994339. A company limited by guarantee. Registered Charity No. 265464 (England & Wales) Registered Charity No. SC037624 (Scotland)

Ulimwenguni kote, karibu nchi zote zinafunga maeneo ya mikutano, pamoja na maeneo ya ibada, kwa kuwa maeneo ya umma yamekuwa maeneo ambayo Covid-19 imeenea haraka. Maeneo haya yanafungwa kwa muda mfupi na ni kwa ajili ya manufaa ya kanisa na jamii. Washirika wa kanisa hawapaswi kuacha wito wa kuabudu na ushirika, lakini kuwa na upendo na kujali ustawi wa wengine, tunapaswa kutimiza sehemu yetu ya kupunguza ugonjwa huo kuenea. Kwa hivyo, ikiwa ibada haziwezi kufanyika katika jengo la mazingira ya kawaida, ni muhimu kufikiria kwa ubunifu kuhusu jinsi 'kanisa' linalovyoonekana wakati wa janga.

**Wafilipi 2:4 (ESV) inatukumbusha, 'Pasiwe na mtu anayetafuta faida yake mwenyewe tu bali faida ya wengine.'**

## Kile Kanisa linaweza na linapaswa kufanya wakati wa mlipuko wa Covid-19

### Kukuza ujumbe sahihi, wa sasa na wazi

Makanisa na viongozi wa kanisa wanapaswa kuwasiliana wazi na jamii yao na kujaribu kuwashawishi kwa wema. Ni muhimu kutoa ujumbe wazi na rahisi kuhusu Covid-19 ambao unaufaa muktadha (km makazi ya mijini na yasiyo rasmi) na kulingana na ushahidi. Tumia njia za ubunifu kukuza ujumbe sahihi, ikiwemo simu, mitandao ya kijamii, video na mabango. Ujumbe unapaswa kujumuisha hatua za usafi zinazopendekezwa ili kuzuia maambukizo
The messages should include the recommended hygiene measures to prevent infection:

- Nawa mikono yako kwa kutumia sabuni mara kwa mara kwa angalau sekunde 20.
- Kohoa na upige chafya kwenye tishu kisha uitupe tishu papo hapo. Ikiwa hakuna tishu, kohoa au upige chafya kwa kujifunika na mkunjo wa kiwiko chako kwenye uso wako.
- Jiepushe kugusa uso wako.



Registered office: 100 Church Road, Teddington TW11 8QE. Registered in England: 994339. A company limited by guarantee. Registered Charity No. 265464 (England & Wales) Registered Charity No. SC037624 (Scotland)

## Kupinga ujumbe wa uwongo na wa kudhuru ili kuepuka kueneza hofu na kuzuia unyanyapaa

Kwa sababu ya hofu au kukosa maarifa, aina nyingi za ujumbe usio sahihi zinasambazwa na kusababisha unyanyapaa na lawama za uwongo zinazosemwa dhidi ya watu walio na virusi hivyo. Watu wanaweza kukosa kuelewa jinsi virusi vinavyoenea, na wanaweza kushuku watu wengine bila sababu. Habari zisizo za kweli zinaweza kusababisha kutengwa, uharibifu na kifo. Viongozi wa imani wanapaswa kusikiliza jamii na kugundua ujumbe usio sahihi unaoenezwa na kuhakikisha kuwa wanauzungumzia na kuurekebisha. Hii ni fursa ya kutuliza hofu na kukuza mitazamo na tabia nzuri.

## Kuonyesha tabia salama

Viongozi wa kanisa wanapaswa kuiga tabia ambazo zina uwezo wa kuokoa maisha na kuzuia maambukizo. Wanapaswa **kuongoza kwa kutoa mfano** wa kunawa mikono mara kwa mara, kufuata mwongozo wa kutoakaribiana kimwili. Kadiri idadi ya matukio yanavyoongezeka, watu zaidi wanaweza kuombwa kubaki nyumbani na 'kutokaribianakimwili' na watu wengine. Hii ni muhimu sana ili kupunguza virusi kuenea na viongozi wa kanisa wanaweza kuweka mfano mzuri kwa kufuata miongozo ya afya ya serikali.

## Kujali waumini

Washirika wa kanisa wanaweza kutengwa, kuwa na wasiwasi na hofu. Sio wote wenye uwezo wa kupata maelezo sahihi kuhusu Covid-19. Wanaweza kuhisi huzuni kwa sababu hawakusanyiki na wengine. Tafuta njia za washiriki kuendelea kuwasiliana na kutoa msaada wa kiroho na kutiana moyo. Saidia familia kukuza katika maisha yao ya kiroho kupitia kuomba na kusoma Biblia. Hii inaweza kujumuisha mafunzo ya Biblia nyumbani, kuunda kikundi cha WhatsApp, au kupigiana simu mara kwa mara.

- Endelea kuwasiliana kupitia simu, hasa na wale ambao wanahisi upweke, hawana ufikiaji wa habari za kisasa au wanaoweza kuathirika.
- Weka kikundi cha WhatsApp cha kujitolea kuwaombea watu, kushiriki maneno ya kutia moyo au hata kutuma mahubiri au mawazo ya Kibiblia.
- Shiriki mafunzo ya Biblia ambayo wanafamilia (katika kaya moja) wanaweza kusoma pamoja.



Registered office: 100 Church Road, Teddington TW11 8QE. Registered in England: 994339. A company limited by guarantee. Registered Charity No. 265464 (England & Wales) Registered Charity No. SC037624 (Scotland)

## Kujali jamii, hasa wale wanaoweza kuathirika

Kanisa halipo kujali maslahi yake tu bali kumpenda Mungu na kumpenda Jirani. Wakristo wanapaswa kuiga maisha ya Yesu wakati huu kupitia neno na vitendo, kuzungumza kuhusu na kuishi na tumaini, upendo na kumjali jirani. Hii itaondoa kukata tamaa, hofu na tabia nyingine za kujithuru ambazo tunaweza kuona wakati huu. Wale walio katika hatari ya chini zaidi (vijana na wenye afya) wanaweza kuwatumikia wengine vizuri. Tafuta njia za kuwashirikisha vijana katika mipango ya kupunguza virusi kuenea. Kwa mfano:

- Shiriki maelezo, kama vile maeneo ya kunawa mikono kwenye jamii, au maelezo mengine muhimu.
- Angalia watu wanaoweza kuathirika na waliotengwa ili kuhakikisha wana chakula cha kutosha na mahitaji mengine msingi yameshughulikiwa.
- Kuwashughulikia watu wenye upweke na hofu, kwa mfano, kuanzisha kikundi cha maombi, kutumia simu au mitandao ya kijamii ikiwezekana.
- Zingatia fursa nyingine za kushughulikia ugonjwa huu katika jamii yako (angalia rasilimali zingine hapa chini).

## Wasaidie washirika wa kanisa kutegemea Biblia ili kuunda mitazamo yao na jinsi ya kukabiliana na virusi hivi

Wakati kama huu tunahitaji kuhakikisha kuwa tunazungumza na kutenda kwa njia ya upendo. Biblia inatuonyesha kuwa hatuwezi kuunda uhusiano wa moja kwa moja kati ya dhambi za mtu na misiba inayotokea duniani, ikiwemo Covid-19. Hatuwezi kuwalaumu au kuwashutumu wanaoambukizwa. Lakini Biblia inafundisha kuwa tunaishi katika ulimwengu wenye mahusiano mengi yaliyoharibika ambapo mateso na magonjwa ni sehemu ya maisha yetu. Tunataka watu waone ahadi ya Yesu ya uzima kamili (Yohana 10:10) na tunafanya hivyo kwa kushughulikia mahitaji ya watu katika kila sehemu ya maisha: kimwili, kiroho na kihisia. (Rasilimali hii inaweza kuwa ya msaada: Mtazamo wa Mkristo kuhusu Covid 19)

## Omba Mungu ili Covid-19 ikome

Kanisa limepewa silaha kamili ya Mungu ya kushughulikia maovu ya ulimwengu huu (Waefeso 6:10–20). Tunajua kwamba vita vyetu sio vya mwili bali ni dhidi ya nguvu za ulimwengu huu wa giza na dhidi ya nguvu za kiroho za uovu katika ulimwengu roho' (Waefeso 6:12). Kwa hivyo maombi ni muhimu kwa wakati



Registered office: 100 Church Road, Teddington TW11 8QE. Registered in England: 994339. A company limited by guarantee. Registered Charity No. 265464 (England & Wales) Registered Charity No. SC037624 (Scotland)

tearfund

huu. Yesu anaelewa hofu na wasiwasi wetu na anatuuliza tuzilete kwake kwa maombi (1 Petro 5:7).

## Rasilimali nyingine

- Tearfund Learn: Rasilimali za COVID-19
- Mwongozo wa afya ya umma kuhusu Covid-19 Kumbuka kufuata mwongozo wa serikali yako.
- Pete Greig Maombi ya Usiku na Mchana: Rasilimali ya maombi ya kutafakari



Registered office: 100 Church Road, Teddington TW11 8QE. Registered in England: 994339. A company limited by guarantee. Registered Charity No. 265464 (England & Wales) Registered Charity No. SC037624 (Scotland)